UNITED NATIONS CONFERENCE ON TRADE AND DEVELOPMENT
UNCTAD

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**EMBARGO**

Yaliyomo katika taarifa hii kwa vyombo vya habari na ripoti inayohusiana nyao haipaswi kunukuliwa au kufupishwa katika machapisho, matangazo au vyombo vya habari vya kielektroniki kabla ya tarehe 8 Desemba 2021, 18:00 GMT.

**(13:00 New York, 19:00 Geneva, 23:30 Delhi, 03:00 Tokyo)**

UNCTAD/PRESS/PR/2021/045*
*Asili: Kiingereza*
*Kwa matumizi ya vyombo vya habari. Tafsiri isiyo rasmi.*
*Panapokuwa na tofauti, toleo la Kiingereza ndilo linatumiwa.*

## ENEO HURU LA BIASHARA LA AFRIKA LINAWEZA KUKUZA UCHUMI KWA NJIA JUMUISHI KATIKA BARA, LAKINI LINAHITAJI HATUA ZA KUONGEZA TIJA NA KUPANUA FURSA

- **Chini ya nusu ya nchi za Afrika zimerekodi ukuaji wa kiuchumi jumuishi katika miaka 20 iliyopita, na kuacha 34% ya kaya katika bara zikiishi chini ya mstari wa umaskini wa kimataifa (dola 1.9 kwa siku).**

- **Biashara ya ndani ya Afrika inaweza kuleta ukuaji jumuishi. Kwa sasa iko chini ikiwa 14.4% ya jumla ya mauzo ya nje ya Afrika, lakini uwezo wa sasa wa mauzo ya nje wa bara ambao haujatumiwa unafikia dola bilioni 21.9, sawa na 43% ya mauzo ya nje ya nchi za Afrika.**

*Geneva, 8 Desemba 2021* – Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA) linaweza kupunguza upunguzaji wa ukuaji wa kiuchumi unaochochewa na COVID-19, mwelekeo wa umaskini na ukosefu wa usawa na kuwezesha ukuaji endelevu na shirikishi katika bara hilo ikiwa hatua madhubuti za msaada zinazolenga wanawake, wafanyabiashara vijana na wafanyabiashara wadogo zitachukuliwa, kulingana na **Ripoti ya Maendeleo ya Kiuchumi Barani Africa 2021** ya UNCTAD iliyochapishwa tarehe 8 Desemba.

Ripoti hiyo inaonyesha kuwa sera za biashara pekee haziwezi kusaidia ukuaji wa uchumi jumuishi katika bara la Afrika. Hatua nyingine zinazohitajika ili kuongeza faida zinazowezekana za usambazaji kutokana na ushirikiano wa kikanda na kusaidia kuhakikisha maendeleo shirikishi ni ushirikiano katika kukuza uwekezaji na sera za ushindani, kuharakisha ufadhili wa miundombinu ambayo hurahisisha uhusiano baina ya miji na kuhakikisha usawa wa fursa za kijamii na kiuchumi na rasilimali za uzalishaji.

AfCFTA, ambapo biashara huria ilianza rasmi Januari 2021, ni moja ya miradi kuu ya Ajenda ya 2063 ya Umoja wa Afrika, ambayo inajumuisha malengo mbalimbali ya ukuaji endelevu na shirikishi. Ukuaji wa

---

* **Mawasiliano**: Kitengo cha Mawasiliano na Mahusiano ya Nje cha UNCTAD, +41 22 917 80 33/5549, +41 79 502 43 11, unctadpress@unctad.org, http://unctad.org/press

Ili kupokea nyenzo zetu kwa vyombo vya habari, tafadhali jiandikishe kwa: http://unctad.org/en/Pages/RegisterJournalist.aspx.

uchumi unaweza kujumuisha wote ikiwa tu utapunguza umaskini na ukosefu wa usawa, ripoti hiyo inasema.

"AfCFTA ina uwezo mkubwa wa kuwezesha ukuaji wa uchumi na kubadilisha matarajio ya maendeleo ya bara la Afrika ikiwa hatua za ziada zitachukuliwa ili kufikia na kusambaza kwa haki manufaa yake mengi yanayoweza kutokea, kwani mafanikio hayo hayatakuja moja kwa moja," Katibu Mkuu wa UNCTAD Rebeca Grynspan alisema.

"Umaskini na ukosefu wa usawa sio hali zisizoepukika. Ni matokeo ya maamuzi ya kisiasa na sera za umma. Ripoti hii itasaidia serikali za Afrika na washirika wa maendeleo kutumia vyema AfCFTA ili kukabiliana na umaskini na ukosefu wa usawa ili kuhakikisha mafanikio yanayotarajiwa kutokana na biashara huria yanajumuisha zaidi."

**Ukuaji jumuishi haupatikani katika nchi nyingi za Kiafrika**

Kulingana na ripoti hiyo, ukuaji wa uchumi umekuwa shirikishi katika nchi 17 tu kati ya 49 za Afrika ambapo data za kutosha za kaya za kati ya mwaka wa 2000 na 2020 zinapatikana. Ukuaji wa uchumi umepunguza umaskini barani humo, ripoti hiyo inasema, lakini ukosefu wa usawa umeongezeka katika nchi 18 za Afrika na haujakuwa jumuishi kwa vigezo vyote katika mataifa 14.

Matokeo haya yanaibua swali kuu la jinsi ukuaji wa uchumi kupitia ushirikiano wa kikanda unavyoweza kuchangia katika kupunguza umaskini na kukuza maendeleo jumuishi, lengo kuu la Ajenda 2063.

Ukuaji wa uchumi wa kipekee katika miaka ya 2000 haujaweza kuboresha kwa kiasi kikubwa maisha ya Waafrika wengi, kwani pengo la mapato kati ya matajiri na maskini limeongezeka. Takriban 34% ya kaya za Kiafrika zinaishi chini ya mstari wa umaskini wa kimataifa (dola 1.9 kwa siku), na karibu 40% ya utajiri wote inamilikiwa na takriban 0.0001% ya wakazi wa bara hilo, kulingana na ripoti hiyo.

Janga la COVID-19 limezidisha ukosefu wa usawa na udhaifu wa makundi yaliyotengwa, na kusababisha watu zaidi ya milioni 37 katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kuishi katika umaskini uliokithiri (katika mstari wa umaskini wa dola 1.9 kwa siku).

**Biashara ya ndani ya Afrika inaweza kuleta ukuaji jumuishi**

Ripoti hiyo inasema uwekwaji huru wa biashara, iwe baina ya nchi mbili, kikanda au kimataifa, unahusisha baadhi ya hasara za mapato ya ushuru na una athari za ugawaji upya. Hata hivyo, biashara zaidi ya kimataifa pia inaweza kuzalisha maarifa ya kikanda, ambayo yanaweza kuongeza ufanisi, kueneza teknolojia na kugawanya tena utajiri.

Biashara ya ndani ya Affika kwa sasa iko chini, ikiwa 14.4% ya jumla ya mauzo ya nje ya Afrika. Inajumuisha 61% ya bidhaa zilizochakatwa na zilizochakatwa nusu, hali inayoonyesha manufaa ya juu zaidi kutoka kwa biashara kubwa ya kikanda kwa kuwezesha ukuaji unaoboresha na jumuishi, ripoti hiyo imegundua.

Ripoti hiyo inasema kwamba ukizingatia biashara isiyo rasmi ya katika mipaka, Afrika inarekodi biashara ya ndani ya kanda, hasa katika kilimo.

Biashara isiyo rasmi ya kuvuka mpaka inaweza kuchangia hadi 90% ya mtiririko rasmi wa biashara katika baadhi ya nchi na kuchangia hadi 40% ya jumla ya biashara ndani ya jumuiya za kiuchumi za kikanda kama vile Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA).

Pia biashara hiyo huwa mwajiri wa mwisho wa makundi mengi yaliyowekwa pembeni, na huwa chanzo muhimu cha mapato kwa watu maskini zaidi na makundi yaliyotengwa kama wanawake na vijana.

**Fursa isiyotumika ya dola bilioni 22**

Ripoti hiyo inaweka wazi kwamba uwezo wa sasa wa bara la Afrika wa kuuza bidhaa nje ambao haujatumika unafikia dola bilioni 21.9, sawa na 43% ya mauzo ya nje ya nchi za Afrika. Inasema dola bilioni 9.2 za ziada za uwezo wa mauzo ya nje zinaweza kupatikana kupitia uwekaji huria wa ushuru chini ya AfCFTA katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Ili kutumia uwezo ambao haujatumiwa, vikwazo mbalimbali vya ndani ya Afrika visivyo vya ushuru, ikiwa ni pamoja na hatua za gharama zisizo za ushuru, mapungufu ya miundombinu na mapungufu ya taarifa ya soko, vinahitaji kushughulikiwa na kutatuliwa. Hii inahitaji juhudi za pamoja chini ya AfCFTA.

Ushirikiano wa muda mrefu katika sera za uwekezaji na ushindani utakuwa muhimu ili kukabiliana na utawala wa soko na watendaji wachache na kupunguza vikwazo vya kimuundo na vizuizi vya kuingia sokoni.

Kwa sababu ya kufungwa kwa mipaka kulikosababishwa na janga la COVID-19, watu waliotengwa kama vile wafanyabiashara wanawake wa kuvuka mpaka, watu wenye biashara ndogo ndogo na biashara zisizo rasmi wamekabiliwa na upungufu mkubwa wa akiba zao na kushindwa kukimu mahitaji ya familia zao, ripoti hiyo inasema.

"Hatua zaidi za kusaidia wanawake na vijana katika biashara, biashara ndogo ndogo na nchi zenye maendeleo duni zaidi za Kiafrika zinahitajika ili kufikia AfCFTA shirikishi zaidi," alisema Wamkele Mene, Katibu Mkuu wa Sekretarieti ya AfCFTA.

**Kuhusu UNCTAD**

UNCTAD ni shirika la Umoja wa Mataifa la biashara na maendeleo. Linasaidia nchi zinazoendelea kupata manufaa ya uchumi wa utandawazi kwa haki na kwa ufanisi zaidi na kuziwezesha kukabiliana na vikwazo vinavyoweza kutokana na ushirikiano mkubwa wa kiuchumi.

Linatoa uchambuzi, linaendeleza maelewano na kutoa usaidizi wa kiufundi kwa nchi zinazoendelea ili ziweze kutumia biashara, uwekezaji, fedha na teknolojia kama njia za maendeleo jumuishi na endelevu.

*** ** ***